

**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI**

**THE HANSARD**

**Tuesday, 26<sup>th</sup> July, 2016**

*The House met at the County Assembly Chamber, Malindi Town, at 2.30 p.m.*

*[The Temporary Speaker (Hon. Ms. Ngala) in the Chair]*

**PRAYERS**

**MOTION**

**ADOPTION ON THE REPORT ON LAND BILLS AND ACTS**

**Hon. Muhambi:** Asante sana Madam Speaker kwa kunipatia nafasi hii ya kusoma Mjadala huu. Unasema kwamba;

THAT, this hon. Assembly adopts the Report on the Committee on Lands, Housing and Settlement on Land Bills and Acts seminar held at the Kenya School of Government, Mombasa from 31<sup>st</sup> March to 2<sup>nd</sup> April, 2016 laid on the Table of this hon. House on Tuesday, 21<sup>st</sup> June, 2016.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. Muhambi. Who is the seconder of this Motion?

*(Hon. (Ms.) Tecla stood at her place to second)*

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. (Ms.) Tecla. The Motion is open for debate.

*(Question proposed)*

**Hon. (Ms.) Tecla:** Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Ripoti hii ya Kamati ya Ardhi waliofanya warsha hapo Kenya School of Government Mombasa tarehe 31<sup>st</sup> March to 2<sup>nd</sup> April, 2016. Nimesimama kuunga mkono Ripoti hii kwa sababu swala la ardhi ni swala nyeti katika ukanda wa Pwani kwa jumla. Tuliweza kusoma mambo mengi pale ndani ambayo yanahusisha sehemu za sheria ambazo zinatajikana ziweze kufanyika ndani ya Kaunti ya Kilifi na upande wa Pwani nzima.

Kulikuwa na uonevu mwingi katika siku za nyuma ambapo mashamba yalikuwa yanachukuliwa tu kiholela na hata kwa wakati huu pia japo yamechukuliwa lakini kunazo sheria

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ambazo tungeweza kuziunda na zingeweza kutetea wakaazi walioko katika sehemu ambazo mashamba yaliweza kunyakuliwa.

Ikawa ni bora na vyema kwamba tuweze kupata mambo haya na baada ya hapo tukiwa kama Bunge la Kaunti ya Kilifi tunaweza kukaa na kupanga yote ambayo yanahusiana na mashamba ili kusudi tukomboe zile sehemu ambazo wakati huu japo zina watu wenyewe lakini kwa sababu wengi hawako, ni wale wanaosemekana kuwa *absentee landlords*. Ziko sheria ambazo tukizipitia tunaweza kukomboa haya mashamba na tuweze kuwaweka watu wetu wapate karatasi za kumiliki. Watu wengi ni maskwota katika hizo sehemu ambazo tunakaa. Ni nchi yetu lakini sasa tunakaa kama maskwota lakini wenye makaratasi wako nje. Tukija na hizo sheria zitakuwa zinamwezesha yule mwananchi aweze kumiliki pale mahali. Yule pengine ni karatasi yake pia ni kwamba aombwe na kuelezwa kwamba katika ile miaka ambayo hayuko katika ile ardhi na mwananchi yuko pale anaweza kuruhusika na mwananchi akapata kibali cha kuweza kumiliki pale mahali. Kwa hivyo ninaunga mkono ili kusudi Bunge hili tuweze kuwa pamoja tukaweze kuunga mkono na sheria hizi ziweze kupita. Asante.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. (Ms.) Tecla. Any other contribution? Hon. (Ms.) Sophie.

**Hon. (Ms.) Sophie:** Asante sana mheshimiwa Spika. Pia mimi naunga mkono Ripoti hii ambayo iko mbele yetu na ambayo ilikuwa pale School of Government, Mombasa. Acha niseme kwamba kabla ya uhuru nafikiri sisi tulikuwa tunamilikiwa mashamba yetu na wazungu ambao kweli walikuwa wakoloni wa kufanya watu wetu wa Kenya wakiwa chini yao. Walikuwa ni wabeberu na baada ya uhuru tukaona kwamba ardhi zile zilinyakuliwa tena na mabwenyenye. Kwa hivyo kulikuwa hakuna sheria ambayo inaweza kuongoza kulingana na ardhi na tunaona ardhi nyingi hata huku Pwani utakuta sisi wenyewe tuko lakini hatuwezi kuzimiliki. Nashukuru katiba ilipokuja ilikuja na sheria ambayo inaweza kutusaidia. Sisi watu wa Pwani tunaweza tukafuatilia ardhi zetu ambazo ziko na tukapata vyeti.

Kwa hivyo yale mafundisho yalikuwa mazuri na nikaona kwamba Wapwani wengi wamekuwa maskwota kwa sababu hatukuwa na sheria ambazo zingetusaidia ya kujua kwamba hizi ardhi ni zetu. Sasa naamini kwamba katika Bunge hili tutakapopitisha Ripoti hii tutakuwa na sheria ambazo zitatusaidia na haswa kupata zile ardhi ambazo ziko na tunaziita *absentee landlords*. Hizi ardhi ziko tu lakini wenyewe hawako. Pia utakuta kuna wengine wanatafuta vyeti kwa njia rahisi ambayo wanamiliki hizo ardhi na kufukuza wananchi wetu. Naamini tutakapopitisha Ripoti hii, tutaweza kupata ardhi nyingi ambazo zimenyakuliwa na watu na wanakaa nazo wakisema kwamba ni zao. Tutasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kupata vyeti na hata kumiliki zile ardhi. Asante mheshimiwa Spika na naunga mkono Ripoti hii.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you. Hon. Mlanda.

**Hon. Mlanda:** Thank you madam Speaker for this opportunity. I stand in support of ...

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Sorry, there is an intervention.

#### MOTION FOR ADJOURNMENT UNDER STANDING ORDER 50 (B)

**Hon. Foleni:** Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi nami nasimama kusema kwamba Hoja hii ambayo iko mbele yetu iweze kuahirishwa mpaka siku nyengine kulingana na Kanuni 50(b). Nasema hivyo kwa sababu swala la ardhi kaunti hii ni swala nyeti na kusema kweli hata kama waheshimiwa wamefika kiwango cha kikao lakini naona itakuwa vyema tukipata ile

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kamati yote ambayo ni ya ardhi iko Bungeni ili iwapo kuna mambo yoyote ambayo ni ya utata basi mheshimiwa mwenyekiti na naibu wake waweze kutufafanulia.

Hoja hii mimi siipingi lakini napinga kikao cha leo tukisukume hadi siku nyengine ambapo Bunge hili litakuwa limejaa. Nasema hivyo kwa sababu swala la ardhi ni swala nyeti na ni muhimu kila mheshimiwa aweze kuchangia vilivyo. Asante mheshimiwa Spika.

*(Hon. Bakari stood at his place to second)*

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. Foleni. Hon. Members, there has been a request for adjournment of the debate. I propose the question that the debate be now adjourned. Can we have contributions on that issue?

*(Question proposed)*

**Hon. Bakari:** Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi pia nimesimama kwa nidhamu kuunga mkono kuahirishwa ama kusongezwa mbele kwa Hoja hii kwa sababu swala la ardhi ni swala nyeti. Nikiangalia hivi katika Bunge hili ni kwamba pia ile Ripoti ni wachache ambao wako nayo na wengi wetu hatuna na itakuwa shida kuchangia. Tunataka tukichangia tuchangie kitu ambacho kwamba kinaweza kueleweka ili tunapokipitisha basi kiwe ni kitu ambacho kimepitishwa vyema na kila mbunge ameweza kuelewa kile alichokichangia. Kwa hivyo nimesimama kuunga mkono mheshimiwa Foleni ili tuweze kusongeza mbele hiki kikao kwa wakati unaofaa. Asante sana.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Mheshimiwa Muhambi.

**Hon. Muhambi:** Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama kupinga kuahirishwa kwa Mjadala huu. Nasema hivi kwa sababu kama vile mheshimiwa aliyeleta huu mjadala wa kuahirishwa kama pengine ana swali kama vile alivyodai basi angeuliza na lingeshinda kujibiwa basi hapo ndipo angesema tuahirishe. Hakuna swali alilouliza na anadai tuahirishe, kwa nini? Mimi napinga, asante.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Excuse me; there is an intervention by hon. Foleni.

**Hon. Foleni:** Hon. Madam Speaker, my intention is not to bring down the intention of the Motion. My intention is to have full participation of this Motion when the House is at least a little bit full. Hon. Speaker, I want to say that the hon. Vice Chairperson has an interest in this particular Motion by the virtue of him being the Vice Chairperson of that particular Committee. So, now that he has stood to table this Report before this House, I do not expect him to support the adjournment of this Motion.

So, I wish to reiterate that the hon. Vice Chairperson might be out of order by the virtue of him being the Vice Chairperson of this particular Committee and at the same time contributing towards what I have brought forward. Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Any other contribution from any other person?

**Hon. Mlanda:** Asante mheshimiwa Spika. Ngoja nisimame pia kuunga mkono kuahirishwa kwa Hoja hii kwa sababu wakati nilipokuwa nataka kuunga mkono Mswada huu ilikuwa ni maelezo yaliyoelezwa na yule aliyeeunga mkono Hoja hii. Kwa yale niliyoweza kushika na kunakili kwa akili, ninaunga mkono kwa sababu waheshimiwa wengi hawako na ni

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

waheshimiwa ambao wanawakilisha wadi tofaouti na swala hili la ardhi si swala la sisi tu ambao tuko hapa. Ni wajibu wetu pia kuzungumza kwa niaba yao. Hata hivyo, naona ni sawa waheshimiwa wenzetu wangukuwa hapa kwa ajili ya kuwakilisha Kaunti yetu ya Kilifi itakuwa ni vizuri waweko ili tupate ile taarifa kamili na tukiendelea kujadili tutaona kama kila mtu ana tatizo la ardhi katika sehemu zake. Ingekua vizuri kujadili kwa umoja. Kwa hivyo, nimesimama kuunga mkono kuahirishwa kwa mjadala huu. Asante mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Asante Mheshimiwa Mlanda. Hon. Kaingu.

**Hon. Kaingu:** Asante sana mheshimiwa Spika. Hata mimi nasimama kuunga mkono kuahirishwa kwa kikao hiki kwa sababu kama tujuavyo, Pwani hasa Kaunti ya Kilifi hili swala la ardhi ni donda sugu. Vile ambavyo tunaona hapa sisi waheshimiwa ni kidogo sana. Japo kiwango cha kikao kiko lakini sio kile tunachojua; ndio sababu naamini changizo zitakuwa duni sana. Kwa hivyo kwa sababu ni swala nyeti na linagusa hapa kwetu Kaunti ya Kilifi, ni vizuri tuweze kuahirisha kikao hiki ili tupange siku ambayo waheshimiwa watakuwa wengi na changizo vile vile tunaamini zitakuwa nyingi za mwelekeo wa Kaunti yetu. Kwa hivyo, hata mimi nasimama kuunga mkono Hoja ya kupinga kuendelea kwa Hoja hii.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you. Hon. Mwayaa.

**Hon. Mwayaa:** Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi nasimama kupinga kuahirishwa kwa Ripoti ambayo iko mbele yetu kwa sababu Bunge hili lina sheria zake, na tunaona kiwango cha kikao kiko, Ripoti imetolewa na ikaelezewa na aliyehunguwa mkono. Vile vile mheshimiwa Spika, yule ambaye ameleta Hoja ya kwamba tuahirisha ni wa upande wa wachache katika Bunge hili. Ataleta nani ambaye atafanya Bunge hili lijae ili tuendele? Yeye yuko peke yake na yuko hapa na wale wengi tuko hapa. Mimi naunga mkono wale wengi ambao tuko hapa tuendele ili tuweze kutamatisha Ripoti hii maana kama ni kumtegemea yeye alete mtu hataleta...

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Excuse me, there is an intervention.

**Hon. Mlanda:** Asante Mheshimiwa Spika. Mimi nimesimama kwa Hoja ya nidhamu kupitia yale ambayo mheshimiwa anaongea, kwamba aliyekuwa anaomba kuahirishwa kwa Hoja hii ni kiongozi wa wachache kwa Bunge hili. Naona hiyo si sababu ya mheshimiwa kuomba kuahirishwa; hiyo ni sababu ya kwamba hawezi kufanya waheshimiwa kuja Bunge hili kwa wingi. Naona kama kuna sababu nyengine mheshimiwa angetuelezea mbali na hayo ambayo ametuelezea.

**Hon. Mwayaa:** Asante mheshimiwa Spika. Nilikuwa nataka kuelezea sababu nyenginezo na ilikuwa hiyo ni sababu mojawapo maana kama ni kujaza Bunge hili, yeye ni kiongozi wa wachache na katika Bunge hili letu la Kilifi ni wawili tu. Labda aite huyo mwenzake na hata akija sidhani kama mjadala...

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): There is an intervention from hon. Bakari please.

**Hon. Bakari:** Asante sana mheshimiwa Spika. Nilikuwa nataka kukufahamisha ya kwamba mheshimiwa Foleni alipokuwa amesimama kuahirisha hiki kikao alinukuu zile sheria zetu za Bunge ambazo zinamruhusu yeye ama Bunge hili kujadili ule Mswada ambao ameleta yeye. Kwa hivyo, nilikuwa namfahamisha mheshimiwa kwamba hivi ndivyo ilivyo kwa sababu ametumia kile kifungi cha Kanuni za Bunge. Asante sana.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Sawa. Endelea Mheshimiwa Mwayaa.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. Mwayaa:** Mheshimiwa Spika, niko na akili za kutosha ndio maana watu wa Kayafungo wakanituma hapa. Sasa kama kuna mtu aliyepigiwa kura mahali kwengine anataka kunifahamisha mimi...

*(Laughter)*

...ni kuonekana watu wa Kayafungo walifanya uamuzi ambao ulikuwa sio wa sawa kwa hivyo yaonekana anataka kuniongezea kile kilichoko kwa akili yangu. Mheshimiwa Spika, nasema mjadala uendelee kwa sababu idadi ya kikao iko. Sababu ya pili, aliyelea nimetangulia kusema yeye ni wa wachache Bungeni na tukimtegemea yeye alete watu ataleta yule mwenzake. Naomba Bunge hili liendelee tujadili mambo yetu ya Kilifi na haya mambo ya ardhi ni mambo nyeti ambayo twafaa tuyaanze saa hii.

Mjadala huu hata usipoisha leo sheria inaturuhusu tuweze kuendelea hata kama ni kesho. Kwa nini tuhairishe saa hii? Labda sababu nyingine ije lakini kama ni ya kwamba Bunge lijae, saa hii tayari tuko katika sheria, Bunge limejaa maanake tuko na idadi ya kikao. Nasema tuendelee na tujukumike katika kazi zetu ambazo tunazifanya katika Kaunti ya Kilifi tupate ardhi zetu na tuone mahali ambapo kuna shida tuwe tutaweza kupagatua kama vile ugatuzi unavyosema. Asanteni na naunga mkono tuendelee ili kwamba tusonge mbele na kuona ardhi zile zilizonyakuliwa pengine sheria hii inaweza ikatuokoa kwa njia moja ama nyingine. Asanteni na napinga kuahirishwa na nasema tuendelee kujadili Ripoti hii.

**Hon. Foleni:** Mheshimiwa Spika, naomba mwenzangu ambaye amemaliza kuongea hivi sasa atuelezee kupitia kwa ile Ripoti, ni ukurasa gani, ama ni sura gani, ama ni kifungu kipi kinaonyesha kwamba kuna ardhi fulani, iko wapi na ilinyakuliwa wakati gani ili tuelewe kupitia ile Ripoti? Ili tuelewe kwamba kile ambacho anasema ni cha ukweli na kinaweza kusaidia Bunge hili. La sivyo, Mheshimiwa Spika atoe matamshi hayo. Asante.

**Hon. Mwayaa:** Mheshimiwa Spika, sikuja kwa mtihani mimi...

*(Laughter)*

...nionyeshe kila ukurasa ambao una shamba lililonyakuliwa. Nilikuwa naunga mkono tu Ripoti hii tuendelee na kuijadili. Lakini mheshimiwa ambaye amesema nitaje kila ukurasa ni kama ambaye niko kwa mtihani...

*(Laughter)*

Nasema tuendelee na tuna imani na Kamati ya kwamba tulijadili na wakaona kuna njia fulani ambazo tunaweza tukakomboa ardhi yetu. Hayo ndio nasema tujadili lakini si mambo na kutaja ni ukurasa gani; tujadili Ripoti na tuendelee bali siko kwa mtihani hapa. Napinga na nasema tuendelee kuijadili.

Kulingana na matamshi ambayo yametolewa na aliyeunga mkono Hoja hii, amesema kwamba katika Ripoti ile waliyoijadili waliona kwamba ikipitishwa basi huenda ardhi zile ambazo zilikuwa zimemilikiwa kimakosa, ndivyo nilivyomnukuu yule ambaye ame...na kupitia matamshi hayo nasema kama kuna hali hiyo aliyotuelezea tuendelee ili kuokoa kile ambacho pengine kesho ama kesho kutwa kingekoseka katika jimbo letu la Kilifi. Kama ni mambo ya ukurasa hata Ripoti ile haijawekwa nambari kwenye kurasa. Sijajua kama imewekwa moja au mbili. Kwa hivyo naunga mkono tuendelee.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Hon. Mlanda.

**Hon. Mlanda:** Madam, I was standing on a Point of Order but unfortunately the hon. Member is already seated. If he cannot substantiate then he better withdraw that remark.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): I think that is what we have told him. If he can not substantiate, he withdraws. Hon. Mwayaa, please do that.

**Hon. Mwayaa:** Wacha niyatoe maneno haya kwa sababu nimeambiwa nitaje ukurasa lakini haya ya kwamba tuendelee bado nasimama nayo.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. Mwayaa. Hon. Kambi.

**Hon. Kambi:** Asante. Nasimama kuunga mkono kuahirishwa kwa Ripoti hii. Kusema kweli, mambo ya ardhi sio mambo ya kiongozi wa wachache Bungeni. Mambo ya ardhi ni matatizo ambayo yamekumba wananchi katika Kilifi yetu. Nimesimama kuunga mkono kwa dhati iahirishwe ili wenzetu wawe hapa na tuchangie vizuri. Tuko na maeneo Bunge saba katika Kaunti yetu na kila eneo Bunge lina matatizo ya ardhi. Kwa hivyo, ni muhimu tukiwa na waheshimiwa wenzetu ili tuwe pamoja na tushikane mikono tujadili Hoja hii kwa ubora zaidi ili itusaidie.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Asante Mheshimiwa Kambi. Hon. Chai.

**Hon. Chai:** Asante kwa kunipa nafasi hii ya kusimama na kupinga kwa dhati Hoja ya kusimamisha Mjadala huu. Mimi napinga kwa sababu moja ama nyingine ambazo zitafwata baadaye. Kuikubali hiyo Hoja kama Bunge sio lazima kila mmoja awe yuko hapa na ikiwa wengine hawako haimaanishi kwamba Bunge hili halitajadili Miswada yoyote. Nina uhakika hata wale watakaokuja pia hawataongea kwa niaba yangu wataongea kwa niaba yao.

Hii Ripoti nimesema tuikubali kwa sababu si sheria ambazo watu hawa wa ardhi walienda kutunga ambazo tutakuja kuzipitia mpaka tuone kama zinatufinya ama kutupendele. Kile kitu ambacho nimesoma hapa ni kwamba wamekuja kutupa Ripoti kutokana na masomo waliyopata. Haya ni masomo sio kwamba walienda kutunga sheria. Kwa hivyo, katika ile hali ya kuikubali ni kwamba tuipitishie na kuwashukuru vile walienda kuongeza ujuzi kidogo katika masomo huko *Kenya School of Government, Mombasa* kutoka tarehe ile waliyoenda. Kwa hivyo naona tukisema kwamba hatuukubali mjadala huu kwamba tuahirishe itaonekana kama ambaye tunataka...

*(Hon. Mlanda stood on a Point of Order)*

**Hon. Mlanda:** I stand on a Point of Order Madam Speaker. Is the Member trying to tell us that we cannot differentiate between a Report and...we are aware that this is a Report and that there is no law that says it is a must that we agree with it in this House. Thank you.

**Hon. Chai:** Asante sana Mheshimiwa Spika. Kitu ambacho najaribu kuongea hapa ni kwamba wanakamati walienda kuelezwa zaidi kuhusu sheria sio kwamba walienda kuunda sheria. Kama wangekuwa walienda kutunga sheria tungekuwa tunahojiana kivingine hapa lakini walienda kuelezwa sheria. Kwa hivyo kama tunapinga hii Ripoti, inamaanisha hata tungeletewa Hoja ya kuomba kwenda kufundishwa haya ambayo walifundishwa hapa pia nayo tungepinga wasiende kufundishwa. Nikishika hii Ripoti ambayo imewekwa hapa, Kamati ya Ardhi inatuletea Ripoti ya baada ya mafunzo na sio kufunzwa sheria ama kutengeneza sheria. Nasimama kupinga kabisa kusimamishwa kwa Ripoti hii kuendelea kusomwa.

**Hon. (Ms.) Arafa:** Thank you Madam Speaker. I stand to support the adjournment Motion of the Report on Land, Housing and Settlement. I am not saying that because I just want

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

to oppose the Report. It is a very interesting Report and I would like to hear more from the Members who attended this training. It is very unfortunate Madam Speaker that even the seconder, hon. (Ms.) Tecla, who stood to support this Motion talked about people who grabbed land and people who took land from the locals at the Coast which the Report does not talk about.

So, I am worried that if the people who attended this training are talking of issues which do not appear in this Report, what of the people who did not attend this training? What are we going to contribute on this? I would wish if the whole Committee on Lands will be here in the House then it will be interesting to hear more from them. I can see there is a lot of pending land Bills which are not in the House. We would also want to know from the Lands Committee how far they have reached. What mechanism are they putting in place to make sure that Members at least go through some of them, even if it is a draft? I can see this Report is for a long time ago; March that is when they attended the training.

The Community Land Bill has been in place since 2015. Have they tried to go through it? It talks about issues of community land. I am not opposing the Report but I am interested to know more about the pending Bills and also the Committee to give us more information on the training they attended; it will be good for this House. Rather than for this House to just pass a Report or just...for some of us, this Report was in our pigeon holes before we went for short recess and majority of us are contributing to this Report and we do not have it at hand. It is very unfortunate Madam Speaker. I am supporting the adjournment Motion of this Report and I am very sure that the next time we come we will have very good contributions to make. Thank you very much Madam Speaker.

**Hon. Mwathethe:** Thank you Madam Speaker for also allowing me to air my views in regards to the Motion of adjournment of the debate that is going on. I stand to oppose that we should adjourn the Motion of the adoption of the Report since the reasons being given for the adjournment are very weak.

Madam Speaker, the Standing Orders require that we have a quorum for us to be able to conduct business. The determination of quorum has been done and confirmed. I do not know as to why or how we should adjourn because some people are not here and nobody knows when they will be here. This is not a school whereby when you do not come, you will be canned. Everybody comes here at his or her own choice. So, to say that someone is not here because he is doing something somewhere and we have a quorum but we cannot continue because...

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): There is an intervention from hon. Mlanda.

**Hon. Mlanda:** Thank you Madam Speaker. Hon. Kadenge Mwathethe is referring to some people. Can he clarify which people he is referring to? Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. (Ms.) Ngala): Proceed hon. Mwathethe.

**Hon. Mwathethe:** Of course Madam Speaker when I said some people I meant those of us who are not here and we know where they are, and they are doing the business of this Assembly. If one team is in one corner doing Assembly business, why should the other team be stopped? This is my argument Madam Speaker; our job is not only to come to the Assembly and deliberate from the Chambers. We may be here and another business may be continuing somewhere else as long as they have quorum there. So, to say that we have to adjourn only because our colleagues...it would be biased, Madam Speaker.

Everybody who stands claims that land is a pertinent issue like this, like that but it has to be debated. Then here we have a Motion on land and everybody is going back. This surprises me

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Madam Speaker. I say that we continue with our deliberations because time is not on our side. Next year we are closing business and we have so much on our calendar. Yesterday we adjourned a debate today we are here just to adjourn another debate. That would be a joke Madam Speaker; as long as we have quorum I beg that we continue. Thank you.

*(Question, that the Debate be now adjourned, put and agreed to)*

*(Debate adjourned)*

### **ADJOURNMENT**

In the absence of any other Business I adjourn this House until tomorrow at 2:30 p.m.  
Thank you.

**The House rose at 3.43 p.m.**